**MAZUNGUMZO NA KIKOSI CHA JWTZ KITAKACHOKWENDA DARFUR, SUDAN**
**MSATA, JUMANNE, 31 MACHI 2009**

1. **SHUKRANI.**

2. **UMUHIMU WA SUDAN NA KWA NINI AFRICA NA ULIMWENGU UKAJALI SANA:**

   **[Nchi kubwa kuliko zote Barani; Mchanganyiko wa Makabila, Rangi na Dini. Kiungo baina ya Kaskazini na Kusini] Inapakana na nchi tisa (9) – Central African Republic, Chad, DRC, Eritrea, Ethiopia, Egypt, Kenya, Libya na Uganda.**

3. **MATATIZO YA SUDAN:**

   **Sudan ya Kusini**

   - **Vita na maafa 1950s hadi 1972; 1983 - 2005.**
   - **Mkataba wa CPA baada ya vifo zaidi ya Milioni mbili.**
   - **Makubaliano ya Eastern Sudan**
   - **Moto wa Makumbi – Kordofan.**
   - **Nature ya utawala wa Khartoum.**

4. **DARFUR**

   - **Iko wapi?**
   - **Eneo: kama la Ufaransa [Maili za mraba 190420].**
   - **Watu: zaidi ya Milioni nne – wengi wengine wapo Khartoum.**
   - **Historia: Ilikuwa nchi huru ya Kifalme, ilivamiwa na Misri na kuanzia 1916**

**ilitekwa na Uingereza na Sudan ambayo waliifanya kuwa sehemu ya Sudan.**

- **Mpaka 1989 ilikuwa Jimbo moja. Lakini Khartoum ikaunda states tatu - North Darfur (el Fasher) South Darfur (Nyala) na West Darfur (El Geneina).**

- **Makabila: Fur, Massalit, Zhagawa (5% lakini ndio Warrior Tribe), na Makabila mengi mengine yenye asili ya "Kiarabu" kama vile Rizegat, Bani Halba na Taisha.**

**[Angalizo: Nani ni nani katika Sudan si rahisi kubainisha].**

- **Dini:**

**5. <u>KIINI CHA MATATIZO</u>**

- **Sababu kubwa ni kutelekezwa, kuonewa na kunyanyaswa.**

- **Tatizo la Wakulima na Wafugaji wakati Jangwa linazidi kusonga mbele.**

- **Usambazwaji wa silaha kutokanana vita baina ya Chad na Libya na mapambano ya Kusini mwa Sudan.**

**6. <u>KUANZA KWA MAPAMBANO YA SILAHA</u>**

- **Mashambulizi ya SLM/A yaliongozwa na Abdul Wahid kiwanja cha ndege cha El Fasher.**

**7. <u>MATOKEO YA MAPAMBANO</u>**

- **Zaidi ya watu 200,000 wamefariki ama kutokana na vita au magonjwa/njaa n.k.**

- **2 – 2.5 milion IDPs.**
- **200,000 Wakimbizi**

**8. <u>JUHUDI ZA AU NA JAMII YA KIMATAIFA KUMALIZA MGOGORO</u>**

- **AU mstari wa mbele.**
- **N'djamena Agreement – April 2004.**
- **Addis Ababa Agreement – May 2004.**
- **Abuja Protocol – Novemba 2004 [Baina ya Serikali inayoongozwa na NCP na Vyama vya SLM/A na JEM].**

**<u>Kupelekwa kwa Wanajeshi wa Africa</u>**

- **Maafisa na Askari 2941 - Polisi 815 na kufikia 6171 na Polisi 1560. [Nigeria, Rwanda, South Africa, Senegal, Gambia, Kenya na MILOBS kutoka nchi mbali mbali].**

**9. <u>MAZUNGUMZO YA AMANI – ABUJA (JUNE 2005 – MAY 2006):</u>**

- **Mambo muhimu yaliyojadiliwa na makubaliano ya DPA {Power sharing; Wealth sharing, Security Arrangements, DDC}.**
- **Walioweka saini: GOS na SLM/MM.**
- **Kwa nini JEM na SLM/AW hawakusaini?**
- **Nani aliyeshiriki katika mchakato wote [UN, LAS, EU, USA, UK, France, Norway, Canada, Netherlands na wengineo].**
- **Nchi za jirani - Chad, Eritrea, Egypt na Libya.**

- **Faida na hasara za DPA.**

**10. MGAWANYIKO WA VYAMA VYA WAASI NA TAATHIRA YAKE**

- **SLM na JEM ndio Vyama vikubwa.**
- **SLM ilianza kugawanyika Haskanita (2005).**
- **Baada ya Abuja mpasuko uliendelea kufikia vyama (Makundi) 20 au zaidi miongoni mwa vyama maarufu ni pamoja na:-**

| | | |
|---|---|---|
| **SLM/A Mini** | **-** | **Mini Minawi** |
| **JEM** | **-** | **Dr. Khalil Ibrahim** |
| **SLM/Abdul Wahid** | **-** | **Abdul Wahid Nour** |
| **SLM/A Freewill** | **-** | **Dr. Adurahman Moussa** |
| **URF (United Resistance Front)** | **-** | **Bakari Abu Garda** |
| **SLM/Unity** | **-** | **Abdallah Yahya** |
| **SLM/Peace** | **-** | **Ibrahim Maibo** |
| **JEM/Peace wing** | **-** | **Abdurisha Abdurahman** |
| **SLA/AS** | **-** | **Abdul Shafi** |
| **JEM/Collectiv** | **-** | **Bahar Idris Abu Garda** |
| **JEM /AZRA** | **-** | **Idriss Ibrahim Arzaq** |

- **Sera ya GOS au angalau baadhi ya viongozi wake kusambaratisha vyama vya waasi.**
- **Kutokuwepo credible force ya kutekeleza makubaliano kulizidi kuzorotesha hali.**

**11. AU/UN LEVEL CONSULTATIONS ADDIS ABABA 16 NOVEMBA 2006**

**Maamuzi:**

**(a) Ceasefire.**

(b) **AU/UN Hybrid Force**

(c) **Appointment of Salim and Eliasson "to re-energize the Political Process".**

12. **AZIMIO NAMBARI 1769 LA 31 JULAI 2007**

- **Kutekeleza DPA.**
- **Kulinda Wananchi wa Darfur.**
- **Kuwalinda Wafanyakazi wa UN n.k.**

**Utekelezaji: Lengo ni Makamanda na Wapiganaji 26,000pamoja na Polisi. Mpaka sasa na 12,000 tu walioko kwenye Midani.**

- **Matatizo ya logistic hasa ndege za helicopters za ushambulizi.**

13. **KUIMARISHA MCHAKATO WA KISIASA**

- **Juhudi zangu na Eliasson za miezi 18. (k.m. Mkutano wa Arusha August 2007; kutembelea na kuzungumza na Vikundi katika maeneo ya mapambano, kutanua wigo wa kushauriana na Vyama vya siasa, Taasisi zisizokuwa za Serikali.**
- **Kuendelea mazungumzo na serikali.**
- **Uamuzi wetu wa kupendekeza Mwakilishi mmoja tu kwa niaba ya AU/UN.**
- **Uteuzi wa Djibril Bassole.**

14. **MCHANGO WA REGIONAL ACTORS**

- **Uhusiano wa Chad na Sudan na waasi wao.**
- **Eritrea**
- **Libya**
- **Egypt**
- **Je tulikuwa tunaimba wimbo mmoja?**

15. **MCHANGO NA MATATIZO YA INTERNATIONAL ACTORS.**

16. **TAATHIRA YA HATI YA MAHAKAMA YA ICC YA KUTAKA RAIS AL BASHIR AKAMATWE**
    - **Kwa nini Afrika inapinga.**
    - **Nini taathira ya uamuzi wa Prosecutor Ocampo na Mahakama ya ICC.**
    - **Maisha ya IDPs na Wakimbizi yanazidi kuzorota [Mashirika 13 yamefukuzwa].**

17. **HALI YA USALAMA**
    - **Imezidi kuwa mbaya kutokana na ICC.**
    - **UNAMID bado kukamilika, lakini hata itakapokamilika itapatwa na matatizo mengi kwa vile bado hakuna makubaliano ya Amani.**
    - **Tatizo la criminal gangs, Utekaji nyara, wizi, mauaji.**
    - **Tatizo sugu la Janjaweed na vikundi vingine vya Militia.**
    - **Mgongano wa vikundi mbali mbali.**
    - **Vuguvugu na mapambano ya Kikabila.**

18. **NGUVU ZA VYAMA:**

    **Vikubwa ni Vitatu**

    **(i) JEM - Ina nguvu za kijeshi lakini haina effective control wala haina support kubwa ya population.**

**(ii) SLM/AW -** **Inaungwa na watu wengi hasa katika Makambi lakini Kiongozi wake haonekani kwamba anataka mazungumzo ya Amani. Pia hawana nguvu za kijeshi.**

**(iii) SLM/Unity -** **Ina nguvu kiasi za Kijeshi.**

**N.B: Vikundi mbali mbali vya SLM ukiwacha kile kinachoongozwa na Abdul Wahid vinashutumiwa kuwa ni vya ki-Zhagawa tu.**

**19. TUNAKWENDA WAPI KATIKA MCHAKATO WA AMANI?**

- **Initiative ya Qatar na mustakabali na matatizo yake.**
- **Juhudi za kutafuta Amani lazima ziendelee.**

**20. USHAURI KWA TANBAT - 1**

- **Watambue kuwa hali ni ngumu.**
- **Ni hali ya "Mapambano" kwa maana hujma za stray elements zitaweza kutokea wakati wowote.**
- **Wawe Imara na Vigilant wakati wowote.**
- **Kwa maneno na vitendo wasionekane wanapendelea upande wowote.**
- **Nidhamu ya hali ya juu.**
- **Mission yao ni muhimu, inathaminiwa na inatekelezeka.**